- Leseni hai ya kukusanya mazao ya uvuvi iliyotolewa na Wilaya au Manispaa,
- Fomu ya maombi ya leseni ya kujishughulisha na biashara ya mazao ya uvuvi, Form 3 (c) (Kanuni za uvuvi za 2009, Kanuni 13(2)(a),
- Fomu ya maombi ya ujenzi/ ukarabati/kurithi eneo la kuchakatia, Fomu 5, (Kanuni za uvuvi za 2009, Kanuni 77(1), 80(1) na 81(1)),
- Leseni hai ya Biashara inayotolewa chini ya Sheria ya kutoa leseni za Biashara (Business Licensing Act), (Kanuni za uvuvi za 2009, Kanuni 14),
- Tax Identification Number,
- Uthibitisho wa uraia (hati ya kusafiria au cheti cha kuzaliwa) wa mmiliki/wamiliki wa kampuni,
- *Certificate of Registration and Extract from Register, or*
- *Memorandum of Understanding and Articles of Associations,*
- *Certificate of Incorporation*,

**NB:** Maelezo ya nyongeza kwa muombaji/waombaji ambao sio raia wa Tanzania,

- Project write up & feasibility study (*endapo andiko hili la mradi likiridhiwa na Wizara/Idara ya Uvuvi utatakiwa kuwasilisha nyaraka zifuatazo)*
    - EIA report,
    - TIC certificate,
    - Taarifa ya tathimini ya athari za kimazingira (environment impact assesment report)
    - Kibali hai cha kufanya kazi nchini (Valid work permit) na,
    - A proof on the value of physical environment relevant to fisheries activities.

Wizara inazidi kuwakumbusha wadau wote wa uvuvi kuwa kwa mujibu wa Sheria ya uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009 "leseni zote zinafikia ukomo wake kila tarehe 31 Disemba ya kila mwaka na kuhuwishwa kwa hiyari kufikia tarehe 30 Machi ya mwaka unaofuata zaidi ya hapo mteja atalazimika kulipa faini ya 50% ya gharama za leseni husika isipokuwa leseni za uvuvi wa burudani".


Kimeandaliwa na
Wizara ya Mifugo na Uvuvi,
Sekta ya Uvuvi,
Idara ya Utafiti, Mafunzo na Ungani,
S. L. P 2847,
40487 DODOMA,

Simu: +255 26 2322613
Nukushi: +255 26 2322613

# JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

### SEKTA YA UVUVI



# UTARATIBU WA KUPATA LESENI ZA SHUGHULI MBALIMBALI ZA UVUVI

Wizara ya Mifugo na Uvuvi,
Sekta ya Uvuvi,
Idara ya Utafiti, Mafunzo na Ugani
S. L. P 2847,
DODOMA,

**TARATIBU ZA KUPATA LESENI ZA UVUVI TANZANIA NA UMUHIMU WAKE**

1. **Utangulizi**

Leseni zote za uvuvi Tanzania Bara zinatolewa chini ya Sheria ya uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na Kanuni za uvuvi za mwaka 2009 (G.N. Na. 308 ya 28/8/2009). Leseni za uvuvi hutolewa kwa mujibu wa sheria na kanuni za uvuvi kama ifuatavyo:-

- leseni za vyombo vya uvuvi ,
- leseni za kujishughulisha na biashara ya kuuza mazao ya uvuvi,

Aidha, utolewaji wa leseni hizi umegawanywa katika sehemu kuu mbili (2)

**1.1 Leseni zinazotolewa na Halmashauri za Manispaa na Wilaya** (Local Government Authority). Leseni hizo ni kama ifuatavyo:-

- leseni za vyombo vya uvuvi vyenye urefu wa chini ya mita kumi na moja,
- leseni za kuvua samaki,
- leseni za kujishughulisha na biashara ya kuuza mazao ya uvuvi ndani ya nchi,

**1.2 Leseni zinazotolewa na Serikali kuu** (Central Government). Leseni hizo ni kama ifuatavyo:-

- leseni za vyombo vya uvuvi vyenye urefu zaidi ya mita kumi na moja (11),
- Leseni ya kuvua samaki kwa mmiliki wa chombo cha uvuvi kinachozidi mita 11.
- leseni za uvuvi wa burudani (Sport Fishing licence),
- leseni za kusafirisha mazao ya uvuvi nje ya nchi,
- Leseni za kuingiza samaki nchini, na
- Leseni maalum.

**2. TARATIBU ZA KUPATA LESENI**

**2.1 Leseni za vyombo vya uvuvi vyenye urefu chini ya mita kumi na moja**.

Nyaraka zinazohitzjika ni kama zifuatazo;-

- Fomu ya maombi ya usajili wa chombo iliyopitishwa na BMU au Serikali ya Kijiji, Fomu na. 1 (Kanuni za uvuvi za 2009, Kanuni 4(1) na (4)),
- Fomu ya maombi ya leseni ya chombo, (Fomu 2(a),) iliyojazwa na kupitishwa na afisa uvuvi wa eneo husika (Kanuni za uvuvi za 2009, Kanuni 11(4)),
- Fomu ya maombi ya leseni ya kujishughulisha na biashara ya mazao ya uvuvi iliyojazwa na kupitishwa na afisa uvuvi wa eneo husika, Fomu 3(a), (Kanuni za uvuvi za 2009,
- Cheti hai cha usalama wa chombo (valid certificate of sea worthiness) kinachotolewa na SUMATRA, (Kanuni za uvuvi za 2009, Kanuni 11(1)),

Chombo kilichopatiwa hati ya usajili na kupewa namba, namba hii lazima iandikwe pande zote mbili za chombo kwa gharama za mwenye chombo (Kanuni za uvuvi za 2009, Kanuni 7(3) na (4)).

**2.2 Leseni za vyombo vya uvuvi vyenye urefu zaidi ya mita kumi na moja** (>11m),

Leseni hii inatolewa kulingana na Kanuni za uvuvi za 2009, Kanuni 11(2).

Mahitaji muhimu ni pamoja na;-

- Barua ya utambulisho kutoka kwa Afisa Uvuvi wa Wilaya au Manispaa,
- Cheti cha usajili wa chombo kilichotolewa na afisa uvuvi wa Wilaya au Manispaa husika.
- Fomu ya maombi ya leseni ya chombo, Fomu 2(a) iliyopitishwa na Afisa uvuvi wa Wilaya au Manispaa, (Kanuni za uvuvi za 2009, Kanuni 11(4)),
- Fomu ya maombi ya leseni ya kujishughulisha na biashara ya mazao ya uvuvi, Fomu 3 (a), (Kanuni za uvuvi za 2009,
- Cheti hai cha usalama wa chombo (valid certificate of sea worthiness) kinachotolewa na SUMATRA, (Kanuni za uvuvi za 2009, Kanuni 11(1)),

**2.3 leseni za uvuvi wa burudani (Sport Fishing licence)**

Leseni hizi zinatolewa kulingana na Kanuni za uvuvi za 2009, Kanuni 18 (3).

Mahitaji muhimu ni pamoja na;-

- Barua ya utambulisho kutoka kwa Afisa Uvuvi wa Wilaya au Manispaa,
- Fomu ya maombi ya usajili wa chombo iliyopitishwa Fomu ya maombi ya leseni ya kuvua (Fomu 3 (a)) iliyopitishwa na Afisa uvuvi wa Wilaya au Manispaa, (Kanuni za uvuvi za 2009, Kanuni 13 (2) (a)),
- Uthibitisho wa uraia (cheti cha kuzaliwa au hati ya kusafiria "*passport*",
- Kibali hai cha kufanya kazi nchini (*valid work permit*) kwa muombaji ambae siyo raia wa Tanzania, (Kanuni za uvuvi za 2009, Kanuni 13 (2)(b).

**2.4 Leseni za kujishulisha na biashara ya mazao ya uvuvi ndani ya nchi.**

Leseni hii inatolewa kulingana na Kanuni za uvuvi za 2009, Kanuni 13(1)(a), (b) na (c). Mahitaji muhimu ni pamoja na;-

- Fomu ya maombi ya leseni ya kujishughulisha na biashara ya mazao ya uvuvi, Fomu 3(a), (Kanuni za uvuvi za 2009, Kanuni 13(2)(a).
- Leseni hai ya Biashara inayotolewa chini ya Sheria ya kutoa leseni za Biashara (Business Licensing Act), (Kanuni za uvuvi za 2009, Kanuni 14)

**2.5 Leseni za kujishughulisha na biashara ya kuuza mazao ya uvuvi nje ya nchi**, leseni hii inatolewa kulingana na Kanuni za uvuvi za 2009, Kanuni 13 (3).

Mahitaji muhimu kwa raia wa Tanzania;-

- barua ya utambulisho kutoka kwa Afisa uvuvi wa Wilaya au Manispaa,
- Barua ya muombaji,